# Makete DC Habari

Karibu uwekeze Makete

Februali 2023

## Watumishi wa Serikali waaswa kuzingatia maadili ya Umma Usiri wa Taarifa

Naibu Waziri Mhe. Deogratius Ndejembi



Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Makete Mhe. Juma Sweda, Kulia kwake ni Aliyekuwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi, akifuatiwa na Mbunge Jimbo la Makete Mhe. Festo Sanga na Mkurugenzi Mtendaji H/w Makete William Makufwe akiwaeleza jambo kuhusu Miradi ya TASAF alipotembelea shule ya Msingi Tandala.



Diwani aomba Kituo cha Polisi Kitulo



***Serikali yakabidhi Pikipiki 7 kwa Watendaji wa Kata Makete***

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi anazungumza na Watumishi Halmashauri ya Wilaya ya Makete huku akisikiliza changamoto zao na kuhimiza utumishi uliotukuka kwa wananchi wa Umma

Katika Kikao hicho Mhe. Ndejembi amewasihi watumishi kutofanya kazi kwa Watsap, SMS na njia ambazo sio sahihi na kuzingatia utaratibu wa Kiserikali kufanya kazi kwa Maandishi ili kupunguza malalamiko huku akitaka waajiri kuacha kuonea watumishi badala yake wawasaidie pale wanapopelekewa changamoto na kutenda haki

Kikao hicho kimefanyika ukumbi wa Halmashauri Februali 20, 2023 naa kuhudhuriwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Makete Clement Ngajilo, Mkuu wa Wilaya Mhe. Juma Sweda, Mbunge Jimbo la Makete Mhe. Festo Sanga pamoja na watumishi kutoka kada mbalimbali Wilayani hapa.




Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi, akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya Makete kwenye ukumbi wa Halmashauri Mwishoni mwa mwezi wa pili, 2023.

## Kitulo waomba Kituo cha Polisi



***Wananchi wa Kijiji cha Ujuni wakiwa kwenye Mkutano na Mbunge Jimbo la Makete Mhe. Festo Sanga***

Wananchi wa Kijiji cha Ujuni na Nkenja Kata ya Kitulo Wilaya ya Makete wameiomba Serikali kuwajengea Kituo cha Polisi kwa lengo la kuongeza ulinzi kwa Wananchi wa eneo hilo kulingana na kuwepo mwingiliano mkubwa wa wageni.

Mbele ya Barazala Madiwani, Mheshimiwa Diwani Kata ya Kitulo Abel Mahenge (Sulemongo) amesisitiza umuhimu wa kujengwa Kituo cha Polisi katika Kata hiyo ambayo kwa sasa ina Polisi Jamii.

Wakiwa kwenye Mkutano wa Kijiji cha Ujuni na Mbunge wa Jimbo la Makete Mhe. Festo Sanga Februali 22, 2023 wananchi hao wamesema kufuatia kuwepo na mwingiliano mkubwa wa watu kwenye kijiji hicho wanaomba uwepo wa Kituo cha Polisi ili kuweza kudhibiti matukio mbalimbali yanayoweza kujitokeza.



***Diwani Kata ya Kitulo Mhe. Abeli Mahenge akiwasilisha ombi la Wananchi wa Kata yake mbele ya Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Makete.***

## *Changamkieni Fursa ya Mikopo-Diwani Viti maalumu Tarafa ya Magoma*

Diwani wa viti maalumu tarafa ya Magoma Nikutusya Fungo amewata wananawake na vijana wilayani Makete kuchangamkia fursa ya mikopo yenye Riba nafuu inayotolewa na Serikali ili wajikwamue kiuchumi.

Nikutusya amesema hayo Februali 21, 2023 akiwa kata ya Iniho wakati wa zoezi maalumu la wataalamu kutoka ofisi ya maendeleo ya jamii wilaya ambao wanazungukia kata zote za wilaya ya Makete kutoa elimu kuhusu mikopo inayotolewa na Serikali kwenda kwa vijana na akina mama pamoja na mtu binafsi yenye riba nafuu.

Diwani huyo amesema riba ya mikopo hiyo ni hafuu sana huku akisisitiza wanawake na vijana kujitokeza kwa wingi kupata mikopo hiyo ili waweze kujikwamua kiuchumi

Baadhi ya wananchi walio jitokeza kusikiliza elimu hiyo wamekiri kuelewa nakwamba awali kulikua na ufinyu wa maelekezo kwenye Jamii kuhusu mikopo inayotolewa na Serikali tena yenye riba nafuu kwa akina mama na vijana

Henri Nyigu ni Afisa Maendeleo amesema Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na makundi maalumu ambayo yenyewe inatoa mikopo kwa wanawake , pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana inatoa mikopo kwa ajili ya vijana, hivyo Wizara zote sasa zimekuja na fursa ya mikopo yenye riba nafuu asilimia 4 kwa akina mama na asilimia 5 kwa vijana hivyo wananchi wachangamkie fursa hiyo.



***Diwani wa Viti Maalumu Tarafa ya Magoma Mheshimiwa Nikutusya Fungo.***

# *Ziara ya Kikazi na Mafunzo Wilaya ya Njombe kuleta Chachu ya ubunifu wa Miradi Halmashauri ya Wilaya ya Makete.*




Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala Wilaya ya Makete imetembelea ujenzi wa Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na nyumba ya Mtumishi inayojengwa Kata ya Kidegembye tarehe 14/02/2023 kwa lengo la kujifunza utekelezaji na usimamizi wa miradi hiyo.

Mradi wa Jengo hilo unajengwa kwa Bilioni mbili na Milioni 900 na nyumba ya Mtumishi kwa zaidi ya Milioni 150.

Katika Ziara hiyo ya Mafunzo Wajumbe wa Kamati hiyo wameambatana na wataalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Makete wamepokelewa na Baadhi ya Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.



***Kamati ya Fedha ikiwa kwenye Ziara ya Mafunzo kiwanda cha kutengeneza Tofali kinachomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe***

Waheshimiwa Madiwani Halmashauri ya Wilaya Makete kupitia Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala imefanya ziara ya mafunzo katika miradi mbalimbali inayotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe

Kamati hiyo imetembelea mradi wa Kiwanda cha kuzalisha Tofali ambapo Halmashauri ya Wilaya Njombe imefanikiwa kuuendeshaa mradi huo tangu mwaka 2019 mpaka sasa

Ikumbwe mwishoni mwa mwaka jana 2022 Halmashauri ya Wilaya ya Makete ilianzisha mradi wa Kufyatua tofali ambapo mradi huo unaendelea vizuri mpaka sasa.

# Madiwani wapongeza ujenzi wa Kituo cha Afya Mbalatse



Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala imeridhishwa na ujenzi Kituo cha Afya Mbalatse kinachojengwa kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo mpaka kukamilika kwake inatarajiwa kugharimu Milioni 400 na fedha zote zimeshatolewa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Makete Mhe. Hawa Kader amesema "tuwapongeze waheshimiwa Madiwani, Mkurugenzi, wakuu wa Idara na Divisheni kwa ushirikiano na kuamua kituo cha Afya kijengwe Mbalatse "

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Albert Msemo amesema kupitia mapato ya ndani Halmashauri imetenga fedha Milioni 400 kwa ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Afya na Maendeleo yake ni mazuri.

"Ujenzi wa Kituo hiki utapunguza adha ya wananchi kusafiri umbali mrefu zaidi ya Kilomita 50 kufuata huduma za Afya na kuokoa maisha ya wanawake na watoto"

Mganga Mkuu Wilaya ya Makete Ligobert Kalisa amewapongeza wananchi wa Kata ya Mbalatse kwa namna wanavyojitolea katika shughuli za Maendeleo ikiwemo kutoa nguvu kazi kushiriki kwenye ujenzi huo.



***Kamati ya Fedha, Mipango na Utawala ikiwa nje ya Majengo Kituo cha Afya Mbalatse ikipokea taarifa ya mradi kutoka kwa Mtendaji wa Kata ya Mbalatse Evelina Sanga***

# Miradi ya Maji ya Bilioni 2.2 yasainiwa Makete



***Wakandarasi walioshinda tenda ya Kujenga Miradi ya Maji Maeneo mbalimbali Wilayani Maket wakisaini Mikataba ya utekelezaji wa Miradi hiyo na Meneja wa RUWASA Mkoa wa Njombe na Wilaya ya Makete, tukio hilo limefanyika Kijiji cha Mfumbi Kata ya Mfumbi***

Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imesaini Mikataba ya ujenzi wa Miradi ya Maji vijijini Wilayani Makete yenye thamani ya Zaidi ya Bilioni 2 kwa lengo la kuondokana na uhaba wa Maji katika maeneo yote ya Wilaya.

Miradi hiyo imesainiwa Februali 21,2023 Kijiji cha Mfumbi mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Makete Mhe. Juma Sweda, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Makete Clement Ngajilo, Mbunge Jimbo la Makete Mhe. Festo Sanga, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Makete Mhe. Hawa Kader, Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Ndg. William Makufwe na viongozi mbalimbali ngazi ya Tarafa, Kata na Vijiji.

Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Usalimwani-Mfumbi wenye thamani ya zaidi ya shilingi Milioni 700, Ujuni-Nkenja wenye thamani zaidi ya shilingi Milioni 800 na mradi wa Kidope-Madihani wenye thamani ya zaidi ya shilingi Milioni 600.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Njombe Mhandisi Sadick Chakka amesema Wilaya ya Makete inajumla ya vyanzo vya maji (Intake) 67 ambapo ndio vyanzo vikuu vya maji yanayotumika kwa skimu za Maji zilizopo. Matenki ya kuhifadhia maji 90 yenye ujazo kati ya Lita 25,000 na 200,000, Vituo vya kuchotea maji 1722 na mtandao wa mabomba unaokadiriwa kuwa na urefu wa Kilomita 539.1

Meneja wa Wakala wa maji safi na usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Makete Mhandisi Innocent Lyamuya amesema wamejipanga kuhakikisha wananchi Wilayani Makete wanapata maji kwa zaidi ya 90%.
Mhandisi Lyamuya amesema Serikali kupitia Wakala wake RUWASA kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 imejipanga kuhakikisha mpaka kufikia mwaka 2025 wananchi wake wawe wanapata maji kwa 85% vijijini na mijini 95% hivyo kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kukabiliana na uhaba wa maji kwa wananchi.
Mpaka kufikia sasa Wananchi wa Wilaya ya Makete zaidi ya 90% wanapata huduma ya maji safi na Salama na matarajio ni kufikisha huduma ya maji kwa wananchi zaidi ya 95%.

# Tani 80 za mbegu ya ngano zapokelewa Makete

Halmashauri ya Wilaya ya Makete imepokea Tani 80 za Mbegu ya Ngano kutoka Wizara ya Kilimo kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo ASA kwa ajili ya kugawa kwa wakulima wa zao hilo Wilayani hapa.

Akizungumza mapema leo kwenye zoezi la makabidhiano ya Mbegu hizo za Ngano Afisa Kilimo kutoka ASA Bi. Aneth Molela amesema Serikali imetoa mbegu hizo kwa lengo la kugawa kwa wakulima ili wazalishe kwa tija na kibiashara zaidi.

Mkuu wa Wilaya ya Makete Mhe. Juma Sweda amesema Wilaya ya Makete itakuwa Wilaya Mama kwa kilimo cha ngano nchini na Hekta zaidi ya 6,000 zimepimwa kwa ajili ya Kilimo cha ngano

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Makete Clement Ngajilo amesema Serikali inafanya yote hayo kuhakikisha inaboresha maisha ya wananchi hususani wakulima wadogo na Kilimo cha ngano itakuwa mkombozi kwa wakulima kwani tayari miundombinu ya Barabara imeanza kufunguka pande zote

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete Mhe. Hawa Kader amempongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara ya Kilimo kwa kuleta mbegu bora kwa wakulima huku akiwasihi wakulima kufanya kilimo cha kisasa

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Makete William Makufwe amesema kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri imetenga fedha zaidi ya Milioni 500 kwa ajili ya kilimo cha ngano na kuwakopesha vijana na wanawake kwa ajili ya kuboresha kilimo cha ngano Wilayani hapa.

Afisa Kilimo Wilaya ya Makete Aniseth Ndunguru amesema Halmashauri imejipanga vizuri kuhakikisha wakulima wananufaika na Kilimo hicho na tayari wameshachukua sampuli za Ardhi kupelekwa maabara ili wakulima waweze kufanya kilimo cha Faida

Baadhi ya wakulima waliofika kupokea Mbegu hizo wameishukuru Serikali ya Jmahuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwajali wakulima na kutambua umuhimu wa Kilimo cha Ngano katika Wilaya ya Makete



***Viongozi Halmashauri ya Wilaya ya Makete wakiongozwa na Mkuu wa Wilalaya Mhe. Juma Sweda aliyeshika Hati ya makabidhiano ya Ngano wakiwa katika mapokezi ya ngano Makao makuu ya Wilaya ya Makete***

# Serikali yakabidhi Pikipiki 7 kwa Watendaji wa Kata Makete

Serikali imewakabidhi Watendaji 7 kati ya 23 kutoka Kata za Wilaya ya Makete wamekabidhiwa pikipiki Februali 23,2023 kwa ajili ya kusimamia shughuli mbalimbali za kimaendeleo katika Kata zao.

Makabidhiano hayo yamefanyika Makao makuu ya Halmashauri na Mbunge Jimbo la Makete Mhe. Festo Sanga Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Makete Clement Ngajilo, Makamu Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya Mhe. Hawa Kader , Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya William Makufwe, Wakuu wa Idara na Divisheni, Maafisa Tarafa, Waheshimiwa Madiwani na Watendaji wa Kata.

Pikipiki hizo zimetolewa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI ambapo Watendaji hao wameshauriwa kuzitunza na zitumike kwa kusudi lililolengwa na Serikali



***Mkurugenzi Mtendaji H/w Makete William Makufwe akimkabidhi ufunguo wa Pikipiki Mtendaji wa Kata ya Mbalatse Bi. Evelina Sanga***



Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Makete William Makufwe amewataka Watendaji hao kutunza Pikipiki hizo ili ziweze kufanya kazi kwa lengo lililokusudiwa na Serikali ili zidumu kwa muda mrefu na ziweze kuongeza mapato ya Serikali kwa kuhakikisha wanatembelea maeneo mbalimbali kukagua miradi ya Serikali na kusimamia ukusanyaji wa Mapato ipasavyo.

# Matukio mbalimbali katika Picha



*Mashimo ya kujenga nguzo za Ghorofa jengo la Utawala lenye thamani ya Bilioni 3 ambapo awamu ya kwanza Serikali imeshatoa fedha Bilioni 1 kuanza ujenzi.*




*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Makete William Makufwe mwenye shati jeupe akiwaongo-za Waheshimiwa Madiwani, Mwenyekiti wa CCM Wilaya walipotembelea kuona maendeleo ya Mradi wa kufyatua Tofali*

# Kitulo FM yaadhimisha Siku ya Redio Duniani




Mchango wa Redio Kitulo Fm kwa Wanawake wajawazito na wanawake waliojifungua watoto Hospitali ya Wilaya ya Makete leo, ambapo Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete Mhe. Hawa Kader akiongozana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri Albert Msemo, Viongozi mbalimbali wa Kata ya Iwawa na Wafanyakazi wa Kitulo FM wametoa zawadi mbalimbali kama Sabuni, Sukari, pampas za watoto, Taulo za Kike, mafuta ya kupaka na kukata Keki kwa pamoja ili kudumisha Upendo na Amani.

Makamu Mwenyekiti Mhe. Hawa Kader amewapongeza wanawake hao kwa kufika Hospitalini hapo kwa wakati sahihi ili kujua Afya zao na waliopata watoto tayari.

Mhe. Kader ameipongeza Redio Kitulo Fm kwa namna inavyohabarisha Jamii na kutambua umuhimu wa kulikumbuka kundi hilo muhimu katika kuongeza uzao katika nchi ya Tanzania.

Mganga Mkuu Wilaya ya Makete Ligobert Kalisa amewashukuru Wafanyakazi wa Kitulo FM kwa moyo wa upendo na kuwaasa wafanyakazi hao kuendelea kutoa elimu ya kudumisha Amani kama ilivyokauli mbiu ya Mwaka huu "Redio na Amani"

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Albert Msemo amewashukuru wadau wote walioungana na Kitulo Fm katika kufanikisha siku hii muhimu kwa michango yao.









***Kikosi cha Wachezaji Timu ya Veterani kwa Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete ambapo Matokeo mpaka dakika 90 zinakamilika ni 1-1 mchezo ulichezwa uwanja wa VETA Makete***




***Kikosi cha Watumishi VeteranWilaya ya Njombe walipofika Makete kucheza na Veterani Watumishi, Mchezo uliochezwa Jumapili tarehe 26 Februali 2023.***

## Kitulo FM yakabidhi Baskeli ya Magurudumu matatu kwa Mlemavu Njombe




*Kitulo FM yakabidhi Baskeli kwa Mlemavu Riziki Mdete mkazi wa Kijiji cha Mamongoro Kata ya Njombe Mjini Wilaya ya Njombe ambaye ni mdau mkubwa wa Redio Kitulo FM*

